# STRAIKA SIMBA USIPIME

>> UK3

JISSNN 2347 - 4189 / Toleo Na. 0006 JUMATATU FEBRUARI 10 , 2025 / Bei Tsh 1,000, Ksh. 100

# SPORT MASTA




## LIGI KUU KUNOGA

# GUU LA MZIZE LINASEMA

>> ANAWABURUZA WENGI KATIKA KUFUMANIA NYAVU

>> UK2



## YANGA SC KUTOTOKA KILELENI

## SIMBA, YANGA WAJUA WABAYA WAO



>> UK2

## MILOUD ANA MIUCHAWI YOTE



>> UK3

# MPANZU ANA HASIRA NAO

# GUU LA MZIZE LINASEMA



NA MWANDISHI WETU

**SIKIA! Clement Mzize ni mshambuliaji namba moja ndani ya kikosi cha Yanga katika eneo la utupiaji akiwa amefunga jumla ya mabao 9 kati ya 42 yaliyofungwa na timu hiyo.**

Mzize anaongoza chati ya watupiaji kwa idadi hiyo akifuatiwa na Elvis Rupia wa Singida Black Stars mwenye mabao 8 kama Leonel Ateba wa Simba.

Katika mabao 9 Mzize hajafunga kwa penalti kwa sababu hakupewa majukumu hayo kwani Yanga ilipata jumla ya penalti 5 mpigaji Aziz Ki aliyepiga nne na Pacome aliyepiga moja.

Ipo wazi kwamba Mzize ndani ya msimu wa 2024/25 ndani ya kikosi cha Yanga ni mshambuliaji wa kwanza kufunga bao alifanya hivyo kwenye mchezo dhidi ya Kagera Sugar uliochezwa Uwanja wa Kaitaba.

Kwenye mchezo huo bao la kwanza lilifungwa na Maxi Nzengeli ambaye huyu ni kiungo mshambuliaji mwenye rekodi ya kuwa mfungaji wa bao la kwanza kwa wachezaji wote wa Yanga.

Mbele ya KenGold Mzize alifunga mabao mawili akifikisha idadi ya mabao 9 ambayo anayo kibindoni na pasi ambazo ametoa zikaleta mabao ni nne.

Yanga ni namba moja kwenye msimamo ikiwa na pointi 45 huku ikifuatiwa na Simba nafasi ya pili na pointi 44 zote zimecheza mechi 17 msimu wa 2024/25.

# MILOUD ANA MAUCHAWI YOTE

NA MWIGA MWIGASI

KOCHA Miloud Hamdi ambaye amechukua mikoba rasmi ya kuifundisha Yanga toka kwa Sead Ramavic aliyeondoka, amesema mashabiki wa timu hiyo watafurahi sana kwa mambo makubwa yanayokuja.

Miloud ambaye tayari yupo Dar es Salaam, amekiri ameiona Yanga na ameifahamu kwani alianza kuifuatilia kitambo na anaamini kile kinachokwenda kufanywa kwa sasa kitawashtua wengi.

Mara alipowasili, kocha huyo alikutana na wachezaji na kuwaambia wazi nini kile anachokitaka kwao, huku akitabanaisha wazi kwake hakuna staa ila kile unachofanya uwanjani ndicho kitakachokugeuza uwe staa kwake.

"Miloud ametua na tayari amekutana na wachezaji wote na kuwaambia matarajio yao kwake, hana mzaha katika hili na amewataka wahakikishe wanaipambania nembo ya Yanga kwa nguvu zote.

"Amezungumza nao kifupi, amewaambia atakutana na mchezaji mmoja mmoja ili kuzungumza naye, ili ajue changamoto ya kila mmoja na amewataka wafunguke kwake," kilisema chanzo chetu.

Miloud mzaliwa wa Algeria mwenye uraia wa Ufaransa, anachukua nafasi ya Ramovic ambaye ameondoka katika kikosi hicho kwa kile kinachodaiwa kupata dili mpya sehemu nyingine.

Ramovic aliwashtua wachezaji akiwaaga rasmi kwamba baada ya mchezo dhidi ya KenGold hataendelea kuwa kocha wa timu hiyo.

"Ni kweli kocha ametuaga baada ya mazoezi kumalizika, kwakweli imetushtua sana, kwanza tulidhani labda amegombana na uongozi lakini ameweka wazi kwamba amepata nafasi ya kwenda kufanya kazi sehemu nyingine," kilipasha chazo chetu.

## Simba, Yanga wajua wabaya wao

NA MWANDISHI WETU

MABINGWA watetezi wa CRDB Federation Cup Yanga SC wamepangwa kucheza na Coastal Union katika hatua ya 32 bora ya miachuano hiyo.

Pia, Simba wao watacheza na TMA Stars ya Championship, huku Azam FC watacheza na Mbeya City ambayo pia, iko Championship.

Tanzania Prisons itacheza dhidi ya Bigman FC, Kagera Sugar dhidi ya Namungo FC, Cosmopolitan dhidi ya KMC FC na Mbeya Kwanza dhidi ya Mambali Ushirikiano.

Nyingine, ni Polisi Tanzania dhidi ya Songea United FC, Kiluvya FC dhidi ya Pamba Jiji FC, Mtibwa Sugar dhidi ya Town Stars FC na JKT Tanzania dhidi ya Biashara United.

Girrafe Academy wamepangwa na Green Warrious FC, Tabora United dhidi ya Transt Camp, Mashujaa dhidi ya Geita Gold, Singida BS dhidi ya Leo Tena huku Fountain Gate wakipangwa dhidi Stand United.

Ratiba hiyo imetokana na droo iliyochezeshwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF)



# MPANZU ANA HASIRA NAO

NA ASHA SEKEFU

WAKATI Simba ikirejea kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Tabora United juzi, winga Ellie Mpanzu ametuma salamu rasmi na kukiri 'Bado Hawajasema'.

Kina nani? Ulizia vyura wanaishi wapi. Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora, Mpanzu alionyesha ubora wake, ambao wanaomjua wanasema hapo ni sawa na asilimia 25 tu ya kile alichofanya ambacho anacho.

Mabao ya Simba katika mchezo huo yalifungwa na Leonel Christian Ateba Mbida aliyefunga mawili na jingine likiwekwa kimiani na Shomari Salum Kapombe.

Lakini achana na walioifunga, ila mfikirie aliyesababisha watu hao wakafunga mabao hayo, ambaye ni Mpanzu aliyechangia mabao yote.

Bao la kwanza Ateba alipokea pasi ya Mpanzu na kufunga dakika ya 12 na la pili akafunga kwa penalti dakika ya 34 kufuatia Mkongo huyo kuangushwa na Faria Jobel Ondongo.

Bao la tatu Ateba alipokea pasi ya Mpanzu tena akiwa kwenye nafasi ya kufunga, lakini akamsetia Kapombe aliyekuwa anatokea nyuma na kufumua shuti lililotinga nyavuni.

Simba inafikisha pointi 43 na kurejea kileleni ikiwazidi pointi moja mabingwa watetezi, Yanga baada ya wote kucheza mechi 16.

Mpanzu mara baada ya mchezo huo hakutaka kuzungumza kwa undani zaidi ya kusema; "bado, bado mtakuja kusema tu". Ikiwa na tafsiri ya mambo mengi ya kile anachokwenda kufanya ndani ya Ligi Kuu.

Haya yanatukia kwa Mpanzu ambaye ameanza kuwatetemesha upande wa pili, huku mstaa wawili ndani ya kikosi cha Simba kinachonolewa na Kocha Fadlu Davids ni balaa zito kwenye mapigo ya penalti kuwa wakishika mpira tu lazima wafunge ikiwa watapewa jukumu la kazi hiyo.

Nyota ambao wamekuwa hatari kwa kupiga penalti ndani ya Simba ni Leonel Ateba na Jean Charles Ahoua waliozikwamisha nyavuni mikwaju yote waliyopata ndani ya kikosi hicho.

Ikumbukwe kwamba kupiga penalti kunahitaji umakini mkubwa kutokana na asilimia kubwa wengi kuhesabu kuwa ni bao, lakini wapo mafundi wakubwa ambao hukosa penalti.

Fadlu pia alikaririwa akisema,m ana Imani kubwa na kikosi chake na kile wanachokifanya kwa sasa ndani ya uwanja, huku akitamba kitaenda kufanya kweli zaidi msimu huu.

# YANGA KUTOTOKA KILELENI

NA ASHA SEKEFU

LAZIMA! Kwa Yanga kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, sasa ni ishara tosha kwa timu pinzani ambazo zipo katika mbio za kuwania taji hilo kuisoma namba. Watalia na kusaga meno.

Sikia. Yanga kwa sasa ipo juu ya msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 45, huku 'wazee wa kubet' Simba wakiwa wanashika nafasi ya pili kwa alama 44 walizojikusanyia. Zote hizi zimecheza michezo 17.

Kukaa kileleni kwa Yanga si kwa bahati mbaya ila juhudi, maarifa na kujituma kwa wachezaji, benchi la ufundi mpaka, viongozi kwa kuiwezesha timu hiyo kufika hapo.

Yanga ikiwa na michezo 17, imefanikiwa kushinda mechi 15 huku ikipoteza miwili na kutikisa nyavu mara 47, huku yenyewe ikiwa imefungwa mabao saba tu, na kuwa na wastani wa mabao ya kufunga na kufungwa 35.

Akizungumzia hilo, Meneja Habari na Mawasiliano Yanga, Ali Kamwe alisema, kwa sasa hakuna tena wa kuiteremsha timu hiyo kutoka ilipokaa na watu wasubiri kubeba kombe mwisho wa msimu.

"Tunachotaka kusema wazi ni kwamba pale sisi tumefika, tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha tunabaki hapo, hawa jamaa wengine watabaki kuisoma namba tu," alisema.

Mashabiki wengi Yanga kwa sasa wameonekana kupagawa na hilo na kutamba, msimu huu utakuwa mwendelezo wa furaha kwao.

## Straika Simba usipime

NA RAJABU KASONGO

MASTAA wawili ndani ya kikosi cha Simba kinachonolewa na Kocha Mkuu, Fadlu Davids ni balaa zito kwenye mapigo ya penalti kuwa wakishika mpira tu lazima wafunge ikiwa watapewa jukumu la kazi hiyo.

Nyota ambao wamekuwa hatari kwa kupiga penalti ndani ya Simba ni Leonel Ateba na Jean Charles Ahoua walizozikwamisha nyavuni mikwaju yote waliyopata ndani ya kikosi hicho.

Ikumbukwe kwamba kupiga penalti kunahitaji umakini mkubwa kutokana na asilimia kubwa wengi kuhesabu kuwa ni bao, lakini wapo mafundi wakubwa ambao hukosa penalti.

Ipo wazi kwamba mkali wa kutuma mguu wa kushoto Bongo, Stephanie Aziz KI ni miongoni mwa nyota ambao kwa msimu wa 2024/25 alikosa penalti ilikuwa kwenye mchezo dhidi ya Tabora United uliochezwa Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam.

Ukirudi kwa Ateba na Ahoua wamekuwa na nyota kali kwenye upande wa mapigo ya adhabu hizo ambapo wote kazi zao zote zilizama kwenye nyavu wakiwapa mateso makipa ndani ya uwanja.

Ateba katupia mabao matano kwenye ligi katika hayo ni mabao matatu kafunga kwa penalti na mawili alikuwa hatari kwenye mwendo ndani ya ligi. Yale yote ya penalti alipopewa alifunga.

Ahoua ni mabao saba kafunga ambapo mguu wake wenye nguvu ni ule wa kulia akifunga yote kwa mguu huo ni mabao matatu kafunga kwa penalti miongoni mwa timu alizofunga ni dhidi ya Dodoma Jiji na JKT Tanzania.

# CRISTIANO RONALDO

## Ajikubali kufanya makubwa



**UNAJUA kila wakati, Cristiano Ronaldo anatuma ujumbe kwa daktari wa timu ya taifa ya Ureno Jose Carlos Noronha, akitaka aambiwe ni kitabu gani anaweza kusoma kuhusu masuala ya sayansi.**

Ronaldo ambaye alizaliwa katika Kisiwa cha Madeira alikuwa tayari ameonyesha kuwa anapenda kusoma, na pia kuvutiwa na masuala ya sayansi, kwa hivyo jambo hilo halikumshangaza Noronha, ambaye amejuana na Ronaldo tangu wakati akiichezea Manchester United.

Daktari huyo, ambaye anaheshimika sana nchini humo ambapo kuna wakati Kocha wa zamani wa United na Chelsea, Jose Mourinho alimwita 'mtu maalumu sana' na kuna wakati alimtaja Ronaldo kama mtu anayependa kujifunza mambo.

"Angeniuliza iwapo kuna makala mapya ya kisayansi angesoma kuhusu lishe au mada tofauti zinazohusiana," alisema Noronha. "Ronaldo ni mtu ambaye hufanya lolote linalohitajika ili kuwa na afya njema ya kimwili na kiakili. Yeye ni mfano mzuri wa kuigwa." Akiwa ametimiza miaka 40 ya kuzaliwa Jumatano wiki hii, Ronaldo analenga kuthibitisha kuwa maisha huanzia katika umri wa miaka 40.

"Nadhani mimi ndiye mchezaji niliyekamilika zaidi kuwahi kutoka katika hii dunia," Alisema kwenye mahojiano na Televisheni moja ya nchini Hispania wiki hii. "Kwa maoni yangu, nadhani ni mimi. Najitahidi kufanya kila kitu kwa njia iliyo sawa katika kandanda.

"Ikiwa unampenda Messi, Pele, Maradona, naelewa na naheshimu msimamo huo lakini kusema kuwa Ronaldo hajakamilika... mimi ndiye niliyekamilika zaidi. Sijamuona mwingine yeyote aliye bora kuliko mimi, na nasema haya kutoka moyoni mwangu."

Mchezaji mwenzake wa zamani Costinha anakumbuka mazungumzo baina yao wakati alipoichezea kwa mara ya kwanza timu ya taifa ya Ureno mwaka 2003 dhidi ya Kazakhstan.

"Aliniambia, 'Costa, Mimi nitacheza kandanda hadi nitakapofikisha miaka 30 kisha nifanye shughuli nyengine tofauti'.

"Siyo tu alitimiza ahadi hiyo, lakini alikwenda mbali zaidi na kufunga mabao mengi zaidi akiwa na miaka hiyo 30 mabao 460. Amefunga mengi zaidi kuliko hata alipokuwa na umri wa miaka ya 20 alipofunga mabao 440.

Hii si kawaida, lakini hakujakuwa na jambo la kawaida kumhusu Ronaldo. Mchezaji huyu anayechezea Al-Nassr kwa sasa anapania kuongeza kiwango chake zaidi akiwa amefikisha umri wa miaka 40 na hajaonesha dalili zozote za kustaafu hivi soka karibuni.

Licha ya mashabiki kuendelea kumkosoa zaidi kutokana na umri wake kwenye mchezo huko, bado anahisi kuna mengi ya kufanikisha.

Miongoni mwa malengo anayoyataka kufikia ni: Kucheza fainali za Kombe la Dunia za mwaka 2026 na kushinda kombe, kufunga mabao 1,000 katika maisha yake ya soka kwa sasa ana magoli 923, kufikisha mechi 250 za kimataifa na Ureno amecheza mechi 217 kufikia sasa

Na kucheza pamoja na mwanae Cristiano Ronaldo Jr, ambaye ana miaka 14 na anacheza timu za vijana za Al-Nassr.

Kwa Ronaldo, wenzake wa Ureno wamejifunza kuwa, kama anavyosema kila mara, 'hakuna kinachoshindikana'.

"Ronaldo hufanya mambo, lakini hufanya akijua kila sababu, na hilo ndilo linanivutia. Nina imani atacheza kwa miaka mingine moja, miwili, au hata mitatu," alisema kocha wake wa zamani wa Al-Nassr, Luis Castro.

"Amefanya nchi yetu ndogo kujulikana duniani kote. Uhakika ni kwamba Ronaldo angefanikisha kila alichofanya, ilikuwa vigumu kutabiri, lakini fikra hiyo ilikuwapo tangu mwanzo.

"Nakumbuka tulikuwa tumejiandaa kuingia uwanjani kukutana na Manchester United (katika mchezo wa kirafiki wa 2003 Alvalade), ambapo timu zote zilisimama kando kando United ikiwa na majina makubwa kama (Ryan) Giggs, Paul Scholes, na (Ruud) Van Nistelrooy," alisema Joao Aroso, ambaye alikuwa kocha wa mazoezi wa mchezo wa mipira wakati huo.

"Ungeweza kutarajia Cristiano, akiwa na umri wa miaka 18 wakati huo, angewaangalia wachezaji hao maarufu. Lakini nakumbuka nilivyomuona Cristiano, akiwa amejikita kabisa kwenye mchezo, bila kuangalia wala kutenguka hakuwaangalia hata kidogo. Hilo linaashiria mengi kuhusu kile alichokuwa akitaka."

Ronaldo alitoka hapo na kwenda Manchester United, kisha Real Madrid na hatimaye Juventus, akishinda tuzo ya Ballon d'Or mara tano na kuwa mchezaji bora zaidi wa Ureno katika historia.

Kocha wa zamani wa utendaji wa Manchester United, Mick Clegg, alisema; "Nimeangalia watu wengi maarufu tangu nifanye kazi na Ronaldo na nadhani Cristiano Ronaldo yupo katika kundi moja na Leonardo da Vinci, Albert Einstein, Isaac Newton, Nikola Tesla, na Stephen Hawking.



# JAY Z ANA VINGI

LOS ANGELES, Marekani

**RAPA wa viwango vya juu, Jay-Z, ameandika historia ya kuwa msanii mwenye tuzo nyingi katika historia ya Grammy.**

**Wikiendi iliyopita, supastaa huyo mwenye mkwanja wa kutosha alibeba tuzo yake ya 25 katika hafla ya msimu wa 47 wa Grammy.**

**Kwa kufanya hivyo, sasa Jay-Z anakuwa amemzidi tuzo moja mshikaji wake, Kanye West, ambaye ana 24.**



# LAMAR ANATAMBA KWA VINGI

LOS ANGELES, Marekani

**LILE bifu kati ya marapa Kendrick Lamar na Drake lilinogeshwa na hafla ya tuzo za Grammy wikiendi iliyopita. Ni baada ya Lamar kumpiku Drake kwa kubeba tuzo.**



**Lamar, kupitia wimbo 'aliom-dis' Drake uitwao 'Not Like Us', alinyakua tuzo tano, ikiwamo ile ya Wimbo Bora wa Hip hop.**


# DAVIDO HANA NOMA

LAGOS, Nigeria

**SUPASTAA wa Lagos, Davido, ameibuka na kumpongeza bibiye anayefanya vizuri katika soko la muziki wa Nigeria, Tems.**

**Katika hafla ya Grammy iliyofanyika Jumapili ya wiki iliyopita, Tems aliibeba tuzo ya Msanii Bora wa Mwaka wa Afrika.**

**Tems aliibeba tuzo hiyo kupitia ngoma yake ya 'Love Me Jeje', akiwapiku mastaa kibao, wakiwamo Yemi Alade na Wizkid.**



# JOSEPH KANIKI 'GOLOTA'



## Mpachikaji mabao Simba aliyewakomoa makipa

**UKIWAULIZA wanachama na mashabiki wa Simba, kuwa miaka ya 2000 mwanzoni ni mpachikaji mabao gani wa timu yao aliyekuwa na mashuti makali, ni dhairi watakuambia kuwa ni Joseph Kaniki au 'Golota' kama mashabiki hao wa Kariakoo, mtaa wa Msimbazi walivyozoea kumwita.**

Mpachikaji mabao huyo aliyekuwa na mwili mkubwa wa kimichezo, alikuwa na kila kitu ambacho mshambuliaji mahiri anatakiwa kuwa navyo, ambavyo si uwezo mkubwa wa kupachika mabao pekee, bali pia mashuti makali na kutumia nguvu pale inapohitajika.

Mkongwe huyo pamoja na kuanza kujulikana kidogo akiwa na timu za mitaani huko Mburahati, lakini umaarufu mkubwa alianza kuupata alipojiunga na Simba mwaka 2000.

Wakati alipojiunga na Simba, miongoni mwa wachezaji aliowakuta na kucheza nao ni Mohamed Mwameja, Ivo Mapunda, George Masatu, Twaha Hamidu 'Noriega', Boniface Pawasa, Amri Said 'Stam', Shekhan Rashid, Athumani Machupa, Said Maulid 'SMG', Issa Manofu na wengine wengi.

Pamoja na 'Golota' kujiunga na Simba mwaka 2000, lakini umaarufu mkubwa katika klabu hiyo alianza kuupata mwaka uliofuata wa 2001, katika mchezo wa watani wa jadi, Simba dhidi ya Yanga.

Katika mchezo wa kwanza wa watani hao wa jadi Simba dhidi ya Yanga, uliochezwa katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru), Septemba 1, 2001, Simba iliibuka kwa ushindi wa bao 1-0 na bao hilo pekee lilifungwa na mshambuliaji huyo Kaniki katika dakika ya 76.

Achilia mbali mchezo huo wa kwanza dhidi ya Yanga, pia nyota huyo alionesha makeke yake katika mchezo wa marudiano, uliochezwa Septemba 30, 2001, katika Uwanja wa CCM Kirumba, mjini Mwanza.

Timu hizo zilitoka sare ya kufungana bao 1-1. Bao pekee la Simba lilifungwa na 'Golota' katika dakika ya 65, huku bao la kusawazisha la Yanga, likifungwa na kiungo mshambuliaji Sekilojo Chambua katika dakika ya 86.

Pia mkongwe huyo 'Golota' alionesha umahiri wake katika mchezo wa marudiano Kombe la Klabu Bingwa Afrika, uliochezwa katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam wakati alipofunga mabao 2-0 dhidi ya Ismailia, lakini mchezo huo uliahirishwa kutokana na mvua kubwa iliyojaza maji uwanjani.

Katika mchezo wa marudiano uliochezwa katika Uwanja huo huo na Simba kuibuka na ushindi wa bao 1-0, lakini bao hilo halikutosha na Simba kuondolewa katika michuano hiyo, kwani katika mchezo wa kwanza uliochezwa mjini Cairo, Misri, Simba ilifungwa mabao 2-0.

Mkongwe huyo alichezea Simba misimu mitatu, huku msimu wa 2002/2003 akihama klabu hiyo na kujiunga na Mtibwa Sugar ya Turiani, Morogoro ambayo alichezea misimu mitano hadi 2006/2007.

Lakini pia nyota huyo kutokana na umahiri mkubwa aliokuwa nao wa kupachika mabao, mwaka 2007 alikuwa katika kikosi cha timu ya taifa, Taifa Stars kilichokuwa kikinolewa Mbrazil Marcio Maximo.

Miongoni mwa wachezaji nyota 'Golota' aliokuwa nao katika timu ya Taifa Stars ni Ivo Mapunda, Shedrack Nsajigwa, Mecki Mexime, Salum Sued, Nadir Haroub 'Cannavaro', Henry Joseph, Athumani Idd 'Chuji', Said Maulid 'SMG', Nizar Khalfan na Renatus Njohole.

'Golota' pamoja na kuzichezea kwa mafanikio Simba na Mtibwa Sugar, pia amezichezea timu kadhaa nchini Sweden, kabla ya kustaafu kucheza soka ya ushindani mwaka 2018.



# NADIR HAROUB HAKUACHA MRITHI?

THOBIAS Nkoma, marehemu Lila Shomari, Athumani Juma Chama, Athuman Maulid "Big Man", Twalib Hilal, Isihaka Hassan "Chukwu", Allan Shomari, Leodgar Tenga, Jellah Mtagwa na wengine wengi tu.




Hao ni mabeki wa Yanga, Simba na Pan African enzi za mwanzoni mpaka katikati ya miaka ya 80. Pamoja na wingi wao, kila mmoja alikuwa na uwezo wa kuitwa kuichezea Taifa Stars.

Ilikuwa ni burudani kwetu sisi watoto wa enzi zile, tulipenda kuwahi asubuhi na mapema pale Posta Mpya kwa ajili ya kununua nakala ya gazeti la Mfanyakazi siku ya Jumamosi kwa ajili ya kujionea ni mabeki gani kati ya hao niliowataja na wengine, ambao walikuwa wamechaguliwa kuichezea Taifa Stars.

Tukishanunua gazeti moja kwa moja macho yetu yanaanzia kwanza katika kurasa za mwisho, ili tutazame picha za wachezaji waliochaguliwa na makocha wa Taifa Stars ya wakati ule, kina Joel Bendera na Jeff Hudson.

Mwanzoni nimewataja mabeki wengi, lakini katika kuitwa kuichezea timu ya Taifa walikuwa wanachukuliwa wachache kati yao, kwani namba zingine za uwanjani zilihitaji wachezaji pia.

Hiyo ndio ilikuwa starehe ya kazi ya kocha wa Taifa Stars, analo kundi kubwa la mabeki wa kati halafu bado kuna mchezaji kama Charles Boniface, mwenye uwezo wa kucheza nafasi zote za nyuma na kiungo wa ulinzi. Kuna fundi Mohamed Adolph Rishard, anaweza kucheza nafasi zote za nyuma na kiungo wa ulinzi.

Mabeki wa kati walikuwepo wa kutosha kabisa na bado makocha walikuwa na uwezo wa kuwatumia wachezaji viraka kama mabeki ikiwa sababu ya kufanya hivyo ingejitokeza. Mfuatiliaji wa soka letu kadri miaka inavyozidi kwenda kwa kasi hupenda kulinganisha kile alichokiona enzi za miaka ya 70, 80 na kile anachokiona leo hii katika viwanja mbalimbali.

naweza akawa anawakera vijana wa kizazi kipya walioketi pembeni yake wakimsikiliza, kwani atajikuta akikereka kadri anavyoziona tofauti nyingi kati ya wakati ule na sasa.

Lakini ukweli wa mambo utakuwa umeshasikika kwa kila mtu, leo hii hali ni tofauti sana na nyakati za kina Jella Mtagwa.

Mabeki wa kati hawaibuki kwa wingi kama zamani, na wakifanikiwa kuchezea timu za ligi kuu, hawana tena ule ugumu kama wale wa miaka ya 80 mwanzoni. Na wenye uwezo wa kucheza soka la kikakamavu, ndio hao ambao wanashindwa kudhibiti washambuliaji wengine ambao kwa enzi zile wala wasingewasumbua mabeki wa kiwango cha kina Isihaka Hassan.

Inasikitisha kuona kuwa Kelvin Yondani na Nadir Cannavaro, mpaka leo hii wanakosa mbadala halisi ambao wataonyesha kwamba limeingia kwenye soka, kundi jingine la wachezaji wenye umri mdogo wenye kufaa kuaminiwa.

Hakuna kitu kinachobakia katika hali ile ile daima dumu, uumbaji wa Mungu umedhihirisha kuwa ni lazima kila kitu kibadilike kutokana na muda unavyokwenda. Kumbuka ile ya Taifa Stars kufungwa magoli 7-0 kule Algeria.

Mabeki wetu wa kati walizidiwa vitu vingi sana na wafungaji wa Algeria, ingawa ukweli huo hatupendi kuuongelea kwa sababu tunazozifahamu sisi wenyewe. Mpenda soka anayewahi nakala ya gazeti lolote lile na kuanza kutazama kwanza kurasa za michezo, atakuwa kachoka kuyaona majina yale yale ya mabeki wa kati.

Tofauti na enzi za utoto wetu, wakati ambapo makocha wa Taifa Stars walikuwa na wigo mpana wa mabeki wa kati. Lile kundi kubwa la mabeki wa kati nililolitaja mwanzoni, hawakuibuka kama uyoga unaojiotea pembeni ya nyumba, walipikwa na makocha wengi ambao hawakuwa na majina wala hawakupata bahati ya kupata mafunzo ya juu ya ufundishaji.

Makocha wa leo ambao ubora wao wa ufundishaji unaboreshwa kupitia mafunzo mbalimbali ya kisasa, wameshaona ni kwa jinsi gani uchache wa mabeki imara wa kati, unavyoziyumbisha klabu zetu na timu ya Taifa.

Uchovu wa miili ya mabeki wetu wa kati huwezi kuuona wakati wa mechi za Ligi Kuu au mashindano mengine ya humu humu nchini, ni wakati wa mechi za kimataifa ndipo unapojionyesha dhahiri.

# WAKIPIGA PENALTI TU, UJUE UMEKUFA!




LONDON, England

UPIGAJI wa mikwaju ya penalti haijawahi kuwa kazi rahisi. Ni kazi iliyowashinda wachezaji wengi, wakiwamo wenye majina makubwa kabisa katika ulimwengu wa soka. Penalti ni tatizo kweli kweli.

Ukiwaweka kando Alan Shearer na Frank Lampard, ambao enzi zao walisifika kwa uwezo wao wa kufunga mabao ya penalti, makala haya yanakuletea wanasoka wengine wenye rekodi mbovu katika shughuli hiyo.

**PAUL POGBA**

Katika penalti zake 15 alizowahi kupiga, Pogba amefunga 10 na kukosa tano. Ni sawa na kukosa asilimia 33 ya mikwaju ya penalti aliyopiga akiwa na klabu za Juventus na Manchester United.



**FRANK RIBERY**

Licha ya uwezo wake mkubwa wa kutengeneza nafasi na kufunga mabao, Ribery hakuwahi kuaminika katika upigaji wa penalti. Kwa penalti zake 17, winga huyo wa zamani wa Real Madrid, Chelsea na Bayern Munich alikosa tano na kupata 12.



**ADRIANO**

Mpachikaji mabao wa zamani wa Inter Milan na timu ya taifa ya Brazil. Alisifika zaidi kwa uwezo wake wa kupiga mashuti yaliyozalisha mabao makali ya nje ya boksi. Katika penalti zake 13, alipata nane na kukosa tano.

**ANTOINE GRIEZMANN**

Ni mmoja ya wapachikaji mabao bora kuwahi kutokea. Hata hivyo, bado Griezmann si mchezaji wa kumtegemea katika penalti. Katika mikwaju yake 27, nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa amekosa mara 11 na kufunga 16.

**RAHEEM STERLING**

Hali ni mbaya zaidi kwa Sterling linapokuja suala la upigaji wa penalti. Nyota huyo wa zamani wa Liverpool, Chelsea na Manchester City ana penalti 10. Katika idadi hiyo, amekosa sita na kufunga nne. Hivi karibuni, alikosa akiwa Arsenal katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Girona.

**OLLIE WATKINS**

Kwa sasa, Watkins ni mshambuliaji tishio Ligi Kuu ya England (EPL) akiwa na kikosi cha Aston Villa. Hata hivyo, nyota huyo raia wa England si wa kutegemewa katika upigaji wa penalti. Katika penalti 12, amekosa sita na kupata sita.



**EDIN DZEKO**

Rekodi zinaonesha kuwa ameshafunga jumla ya mabao 363. Lakini, katika upigaji wa penalti, huwezi kuliweka jina la Dzeko. Katika penalti zake 15, straika huyo wa zamani wa Manchester City amekosa nane na kupata saba.

**ROBERTO BAGGIO**

Wengi watakumbuka makali ya upachikaji mabao aliyowahi kuwa nayo straika huyo wa zamani wa timu ya taifa ya Italia. Hata hivyo, Baggio hakuwa 'mtamu' wa shughuli nzito ya upigaji wa penalti. Katika penalti 34, alikosa 18 na kufunga 16 pekee.

ANDREA PIRLO

Alistaafu soka akiwa ameacha heshima ya kutosha ya upigaji wa faulo. Siyo penalti. Katika penalti 24, kiungo huyo wa zamani wa Juventus na timu ya taifa ya Italia alikosa nane na kupata 16.

**MARIK HAMSIK**

Akiwa na Napoli, Hamski ndiye mchezaji mwenye heshima kubwa klabuni hapo kwa miaka ya hivi karibuni. Katika penalti zake 17, alikosa tisa na kufunga nane pekee. Kwa ufupi, takwimu zinaonesha kuwa huwezi kumtegemea Hamski katika upigaji wa penalti.

# Jamal Musiala:

## Jifanye humjui wala kumfahamu ili akulize



NDANI ya msimu huu, kinda wa Bayern Munich, Jamal Musiala, aliandika historia katika maisha yake ya soka la kulipwa. Alifunga bao pekee katika sekunde ya 15 tu ya mchezo wao wa tatu msimu huu wa Bundesliga.

Ilikuwa pale Bayern ilipoondoka na ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya Holstein Kiel. Mechi hiyo ilichezwa katika Uwanja wa Allianz Arena.

Hata hivyo, Musiala si mchezaji wa kwanza kufunga bao la mapema katika historia ya Ligi Kuu hiyo ya Ujerumani (Bundesliga).

Kwa sasa, rekodi ya bao la mapema katika historia ya Bundesliga inashikiliwa na Kevin Volland. Katika mchezo dhidi ya Bayern uliochezwa Agosti 22, 2015, nyota huyo wa Hoffenheim alitumia sekunde tisa tu kupasia nyavu.

Ni rekodi inayoshikiliwa pia na Karim Bellarabi, ambaye naye alifunga bao la sekunde ya tisa katika mchezo uliozikutanisha BorussiaDortmund na Bayern Leverkusen mwaka 2014.

Mchezaji anayeshika nafasi ya pili katika rekodi ya mabao ya mapema katika historia ya Bundesliga ni Ulf Kirsten. Nyota huyo alipachika bao la sekunde ya 11 katika mchezo Leverkusen na FC Kaiserslautern.

Rekodi hiyo pia inashikwa na Giovane Elber aliyezifumania nyavu katika sekunde ya 11. Alifanya hivyo Desemba Mosi, 1998, mchezo uliozikutanisha Bayern na Hamburger SV.

Wakati huo huo, rekodi hiyo pia ni ya Paul Freier, ambaye naye aliingia kambani katika sekunde ya 11 ya mchezo kati ya Bochum na 1860 Munich. Mechi hiyo mwaka 2003.

Nyota mwingine anayeingia hapa ni Adam Szalai. Alifunga bao la sekunde ya 12, mchezo wa Mainz na Werder Bremen uliochezwa Marchi 30, 2013.

Szalai Zander anaingia pia kwenye orodha hiyo. Zander alipasia nyavu katika sekunde ya 12 ya mchezo kati ya St Pauli na Karlsruher uliochezwa Desemba 4, 1991.

Kwa upande mwingine, lejendari wa Bayern, Lothar Matthaus, naye yumo kwenye rekodi ya kufunga bao la mapema. Alipasia nyavu katika sekunde ya 13 katika mchezo kati ya Bayern na Borussia Monchengladbach. Alifanya hivyo mwaka 1986.

Kiungo wa kimataifa wa Ujerumani, Leon Goretzka, naye anaingia kwenye rekodi hii. Lakini, kwa kiungo huyo, alijifunga katika sekunde 13 ya mchezo wa timu yake ya Bayern dhidi ya Augsburg uliochezwa mwaka 2019.

Katika orodha hiyo, Mohamed Zidan, naye hajakosekana kwenye orodha hii. Alifunga bao la sekunde ya 14 ya mchezo kati ya Werder Bremen na Mainz. Ni mechi ya Bundesliga iliyochezwa mwaka 2006. Ni kama Ronald Worm, aliyefunga bao la sekunde ya 14 katika mchezo kati ya Duisburg na Hamburger SV.



# VICTOR COSTA NAMPOKA:

## BEKI KUBWA LA MAADUI ALIYEPITA SIMBA

UNAPOZUNGUMZIA mabeki bora wa kati waliowahi kutamba hapa nchini kutokana na kucheza kandanda safi na la uhakika, kamwe huwezi kuacha kulitaja jina la Victor Costa au 'Nyumba' kama wapenzi wa soka, hususan wa klabu ya Simba walivyokuwa wakimwita.

Ubora wa beki huyu ulitokana na aina ya uchezaji wake, kwani licha ya kuwa kikwazo kikubwa kwa washambuliaji wasumbufu, pia alikuwa anatumia akili mno, alikuwa na uwezo mkubwa wa kumiliki mpira na kuwageuza kwa kuwapiga chenga washambuliaji katika eneo la hatari.

Pamoja na kutamba akiwa na klabu kadhaa zikiwemo Simba SC na Mtibwa Sugar ya Turiani, Morogoro, pia umahiri wake huo mkubwa aliuonesha katika vipindi kadhaa alipokuwa akichezea timu ya taifa , Taifa Stars.

Costa licha ya kujulikana katika ulimwengu wa soka akiwa na klabu kadhaa Visiwani Zanzibar kama Taifa Jang'ombe na Forodha, lakini alianza kujipatia umaarufu mwaka 2002 akiwa na klabu ya Mtibwa Sugar.

Miongoni mwa wachezaji mahiri aliokuwa nao Mtibwa ni Meck Mexime, Geofrey Magori, Kassim Issa, Alfonce Modest, John Mabula na Hassan Mbaruku.

Nyota huyo akiwa na Mtibwa Sugar mwaka huo wa 2002, kutokana na umahiri mkubwa aliokuwa akiuonesha uwanjani, hususan wa kuwadhibiti washambuliaji wasumbufu, kulimwezesha kuchaguliwa kwa mara ya kwanza kuchezea timu ya taifa, Taifa Stars.

Mkongwe huyo akiwa na timu ya Taifa Stars, huku akicheza vizuri na pacha wake wa kati Boniface Pawasa, ndipo hapo Simba walipomwona na kuvutiwa naye na hatimaye msimu wa 2002/2003 kumsajili katika klabu hiyo yenye maskani yake makuu Kariakoo, mtaa wa Msimbazi.

Akiwa na klabu ya Simba, miongoni mwa wachezaji aliowakuta na kucheza nao ni Juma Kaseja, Said Sued, Ramadhani Waso, Amri Said 'Stam', Boniface Pawasa, Christopher Alex (marehemu), Stephen Mapunda 'Garrincher', Seleman Matola, Athuman Machupa, Emmanuel Gabriel 'Bastituta', Joseph Kaniki 'Golota' na Ulimboka Mwakingwe. Kocha alikuwa ni James Siang'a (marehemu).

Mafanikio makubwa nyota huyo akiwa na klabu hiyo ya Simba mwaka 2003, alikuwa ni miongoni mwa wachezaji walioitoa katika michuano ya Klabu Bingwa Afrika klabu ya Zamalek ya Misri, baada ya kuwafunga mabao 3-2.

Katika michuano hiyo, mchezo wa kwanza uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru) na Simba kuibuka kwa ushindi wa bao 1-0, lililofungwa na mshambuliaji Emmanuel Gabriel 'Bastituta'.

Mchezo wa marudiano ambao ulichezwa Cairo, Misri, Zamalek waliibuka washindi baada ya kuwafunga Simba bao 1-0, hivyo kutokana na ushindi walioupata Simba nyumbani wa bao 1-0 matokeo sasa yakawa ni sare ya bao 1-1.



Na ndipo hapo ile sheria ya kupigiana penalti tano tano ilipotumika na Simba kuibuka na ushindi huo wa mabao 3-2.

Katika mchezo huo wa marudiano, sifa kubwa zilimwendea golikipa wa Simba Juma Kaseja ambaye aliokoa michomo miwili ya penalti.

Pia katika michezo yote miwili ya Simba dhidi ya Zamalek, wa kwanza uliochezwa jijini Dar es Salaam na wa pili uliochezwa mjini Cairo, Misri, Victor alikuwa kikwazo kikubwa mno kwa kuwadhibiti washambuliaji wa Zamalek wasifurukute.

Pamoja na mafanikio hayo, pia mwaka 2004 Victor alikuwa katika kikosi cha Simba kilichotwaa Ubingwa wa Soka Tanzania Bara, bila ya kufungwa hata mchezo mmoja na kocha wa Simba wakati huo alikuwa na Patrick Phiri.

Mkongwe huyo pamoja na kuichezea kwa mafanikio makubwa klabu ya Simba, pia kwa kipindi chote cha miaka mitano kuanzia 2003 hadi 2007, alichoichezea klabu hiyo, pia aliichezea timu ya taifa ya Tanzania Bara 'Taifa Stars'.

Nyota huyo baada ya mkataba wake na Simba kumalizika, alikutana na rungu la kufungiwa miezi sita na Shirikisho la Soka Nchini (TFF), baada ya kusaini timu mbili za Yanga na Simba, lakini alikwenda nchini Msumbiji na mwaka 2011 alirudi nchini na kujiunga na timu yake ya zamani Simba na alikaa nayo hadi alipostaafu kucheza soka la ushindani msimu wa 2012/2013.

# RAMADHANI KILAMBO

## KIFAA KILICHOPITA YANGA

**UNAPOTAJA wachezaji waliokuwa wanacheza nafasi zaidi ya moja uwanjani waliowahi kuichezea klabu ya Yanga miaka ya nyuma, kamwe huwezi kuacha kulitaja jina la Ramadhani Kilambo ambaye ameichezea klabu hiyo yenye maskani yake makuu Kariakoo misimu miwili 1990/1991 hadi 1991/1992.**

Umahiri wa mkongwe huyo ulitokana na aina ya uchezaji wake, kwani wakati wa enzi zake za kucheza soka ya ushindani, alikuwa anacheza kwa umakini mkubwa, huku akijituma katika nafasi yeyote ile, iwe ya ulinzi, kiungo au ya ushambuliaji.

Nyota huyo pamoja na kuanzia kucheza katika timu nyingi ambazo hazikuwa na majina makubwa, lakini alianza kujulikana zaidi msimu wa 1990/1991 alipojiunga na klabu ya Yanga.

Nyota huyo baada ya kujiunga na Yanga miongoni mwa wachezaji aliowakuta na kucheza nao ni Stephen Nemes 'Masajage', Kenneth Mkapa, Godwin Aswile 'Scania', Said Zimbwe (marehemu), Issa Athumani (marehemu), Athumani China, Joseph Machela, Thomas Kipese 'Uncle Thom', Justine Mtekere (marehemu).

Wengine ni Sanifu Lazaro 'Tingisha', Peter Tino, Mohamed Yahaya 'Tostao', Said Sued 'Scud', John Mngazija (marehemu), Willy Mtendamema, Wastara Baribari na Abdallah Selemani 'Kaburu'. Yanga wakati huo ilikuwa ikinolewa na Syllersaid Mziray mbaye hivi sasa ni marehemu.

Mkongwe huyo akiwa na klabu ya Yanga, mechi iliyompandisha chati ilikuwa ni mchezo wa kirafiki wa Kimataifa dhidi ya timu ya Taifa ya Uganda 'The Cranes', uliochezwa katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru) mwaka 1991.

Matokeo ya mchezo huo ambao ulikuwa ni mkali na wa kusisimua kwa muda wote wa dakika 90, yalikuwa ni sare ya bao 1-1. Katika mchezo huo Kilambo alicheza nafasi ya ushambuliaji namba 10, huku akishirikiana vyema na Abdallah 'Kaburu', Sanifu Lazaro 'Tingisha, Wastara Baribari na Abubakar Salum 'Sure Boy'.

Katika mechi hiyo ya kirafiki dhidi ya 'The Cranes', Yanga ilimchezesha beki aliyekuwa Simba wakati huo Deo Njohole 'OCD' akiwa kama mgeni mwalikwa. Njohole aliletwa kucheza katika mechi hiyo ya kirafiki na aliyekuwa mfadhili mkuu wa Yanga wakati huo marehemu Abbas Gulamali.

Msimu wa 1990/1991 wa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara (sasa Ligi Kuu), Yanga dhidi ya Simba, katika michezo yote miwili ambayo Yanga ilishinda bao 1-0 michezo yote, kilambo alikuwa ni miongoni mwa wachezaji wa Yanga waliocheza mechi hizo.

Ikumbukwe kwamba katika michezo yote miwili, bao hilo pekee lilifungwa na mshambuliaji chipukizi wakati huo aliyekuwa anacheza safu ya kati Said Sued 'Scud'.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa katika Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), Jumamosi Mei 18, 1991 na 'Scud' alifunga bao hilo pekee katika dakika ya saba na katika mchezo wa marudiano 'Scud' alifunga bao katika dakika ya 59.

Mwaka 1992, Kilambo alihama Yanga na kujiunga na Reli FC ya Morogoro maarufu 'Kiboko cha Vigogo'. Baada ya kujiunga na Reli, nyota huyo akawa ni miongoni mwa wachezaji wa kutegemewa wa klabu hiyo.

Miongoni mwa wachezaji aliowakuta na kucheza nao ni Mwanamtwa Kiwhelo, Boniface Njohole, Juma Salum, Mbui Yondani, David Mihambo na marehemu Duncun Butinini.

Ramadhani Kilambo, pamoja na kuzichezea Yanga na Reli kwa mafanikio, pia amezichezea klabu kadhaa zikiwemo Chuo Sokoine, Canvas zote za Morogoro na timu ya Mkoa wa Morogoro.





# UMEFIKA WAKATI WA KUPIGANA PINI



**MTU anaweza kushangaa ni kwa nini rundo la viongozi wanaoongozana na timu zetu huko nje huwa hawajifunzi chochote kila mwaka.**

Umakini wa mtu unamfanya ashangazwe ni kwanini kila msimu wakati wa mechi za ugenini za michuano ya ngazi ya Afrika, yanakuwepo mengi ya kujifunza lakini hakuna kipya kinachokuja kuonekana ndani ya timu zetu.

Utalii wa kudumu unakuwa ni sifa ya viongozi wa timu zetu zote, kuanzia ngazi ya taifa mpaka klabu. Wanakwenda nje wakiambatana na mikogo mingi, wanajionea miundo mbinu bora wa klabu kubwa za Afrika, halafu wanarudi nyumbani na kuendelea na maisha ya kawaida.

Hapo unakuwa ukisubiriwa msimu mwingine ili maisha ya mazoea yaweze kuendelea kama ilivyozoeleka. Kile kilichotazamwa na viongozi wa timu zetu huko nje, kinageuka sinema ya bure kwao lakini ni kwa hasara ya kudumaa kwa maendeleo halisi ya klabu wanazoziongoza.

Kiongozi aliyeyaona makubwa yanayoizunguka Al Ahly miaka 20 iliyopita hana tofauti na mwingine aliyeyaona mambo ya kipekee ya MC Alger miaka miwili iliyopita. Tunazungumzia miundombinu.

Tatizo linaweza kuwa juu ya uwezo wa utatuzi wa viongozi wa klabu zetu, lipo kwenye ukosefu wa mtazamo wa usimamiaji wa michezo unaoendana na zama za uwazi wa kimaisha.

Miaka ya nyuma Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na wadau wa michezo, alikuja na mkakati wa kupitia sera nzima ya michezo. Ule ulikuwa ni mwanzo wa mapambano ya kweli yenye nia ya kuingiza uwajibikaji michezoni.

Ukweli klabu zetu zimekuwa na ombwe la uongozi, ambalo linatokana na michezo kuonekana na sehemu tu ya burudani za wanajamii. Kwa michezo kuchukuliwa kama ni mchakato wa kuwapatia watu furaha za jioni wakiwa wametoka kwenye majukumu mengine ya kimaisha, ni hasara ya ukuaji wa sekta nzima ya michezo.

Klabu zetu zimekuwa ni mali ya umma kwa miaka mingi sana, na kila mtu anavichukulia kama sio sehemu ambayo inamhusu kwa asilimia zote mia moja, ikiwa pia kukosekana ukaribu wa Serikali katika usimamiaji wa michakato mingi ya kimichezo.

Timu inakwenda kucheza mechi ya ugenini, fedha nyingi inatengwa kwa matumizi ya huko nje ya nchi. Inarudi nchini na hakuna mwenye kuhoji namna fedha ilivyotumika huko nje.

Ipo kila sababu kwa wizara yenye dhamana ya michezo kutazama hata mahusiano kati ya vyama vya michezo na mashirika wahisani, ambayo ni ya nje ya Tanzania.

Hii ni kwa sababu kuna suala jingine la kulitazama, kwani kuna fedha nyingi ambazo zinakatwa kama makato ya TFF kutoka kwa timu za Ligi Kuu na vile vya Daraja la Kwanza, na zenye zifanyiwe uhakiki ili ijulikane ni namna gani ambavyo haziwezi kuwa chanzo cha hulka za kifisadi.

Fedha za wadhamini pamoja na upatikanaji wa makampuni yenye kupewa nafasi za kudhamini, na huku pia ni muhimu kutazamwa kwa ukaribu. Klabu zetu ni mali ya umma, na kwa sababu hiyo kila anayepewa dhamana anajikuta akiogopa kuwa mbunifu kwa kuogopa kutumia nguvu ambazo baadae zitageuka kuwa majuto kwake.

Lakini kuwa mali ya umma sio dhambi hata kidogo, na dhana nzima ikieleweka vizuri kwa wanajamii, vinaweza kuwa tajiri kuweza kushindana na mazingira halisi ya dunia ya sasa.

Na ni afadhali sana kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inapigana kwa kila njia kuweza kuondokana na dhana ya mali ya umma ni ya kupigwa tu, hivyo hata wenye malengo mabaya na wao wanayo haki ya kudhulumu maendeleo yanayotegemewa.

Ni mwanzo mzuri kwa serikali ambayo imekuja kimkakati zaidi, kwa maana ya kushughulika na mizizi ya matatizo na sio kukata matawi tu halafu ugonjwa unabakia pale pale mwaka nenda mwaka rudi. Kilicho cha wote na chenyewe huhitaji sana nidhamu ya matumizi na mapato.

Kwa klabu zetu kuyafikia maisha halisi wanaoishi wenzetu, mwanzo ni lazima uwe mchungu kwa baadhi ya hulka mbaya za watu walio karibu na michezo.

# HIVI UNAMJUA XAVI AU UNAMSIKIA?

**NI baada ya yale majeraha ya Pep Guardiola ndio kijana akapata nafasi, Toka Barcelona B mpaka kuwa 'Master Tik Tak', si mwingine ni Xavi Hernandez Creus. Huyu ndio yule Xavi, kiungo anayepiga pasi nyingi kuliko timu pinzani na zote zinakamilika.**

Xavi 'maestro' wa mpira dunia haitamsahau, kwani aliisaidia timu kutwaa ubingwa wa ligi mwaka 99 na kutwaa Tuzo ya Mchezaji Bora wa mwaka

Ubora wa Xavi ulionekana mara baada ya kupanda timu ya wakubwa na bosi Juan Laporta na kuwaletea kocha mpya Mdachi Frank Rijkaard, pamoja na mafundi wengine wa mpira kama Deco de Souza, Ronaldinho Gaucho na Samuel Eto'o Fills.

Baada ya kuumia kwa Pep ndipo Xavi ana pata nafasi, lakini Guardiola huyo huyo baada ya kuwa meneja wa FC Barcelona pia anambakisha Xavi klabuni hapo ambae alikua mbioni kuondoka.

Mitaa haitamsahau Xavi ambaye alipiga pasi nyingi sana pale Wembley dhidi ya Alex Ferguson na Manchester United yake na Malaga hawatamsahau kijana aliyepiga pasi nyingi kuzidi timu yake.




The Pass Master Xavi, alivunja record ya kupiga pasi nyingi katika mechi moja akipiga pasi 127, peke yake, kwenye ushindi wa 4-0 wa Ireland Kaskazini na kwenye mechi hiyo alitoa pasi msaada mbili (asist).

Miaka 18 ya mafanikio pale Camp Nou, dunia haitamsahau fundi huyu, kupiga pasi kwake ni furaha zaidi kuliko kufunga ndio maana amecheza mechi 505 na kufunga magoli 58 katika ngazi ya klabu.

Hernandez Xavi, maono zaidi ya yale ya kinyonga, fundi, wa kuutuliza mchezo, ni mmoja wa wachezaji wa kihspania waliopambwa na makombe mengi.

Xavi huyu alifanikiwa kunyanyua ubingwa wa ligi mara 8 na UEFA mara 4 mashindano mawili ya Europa na Kombe la Dunia.

Sijui umwelezeje Xavi namba 6 mgongoni, sura ya kipole, mtaalamu wa kuchungulia mashimo ya uwanja upande wa wapinzani, akili ya mpira, bingwa wa kuuelekeza mpira wapi uende, akiwa na pacha wake Andres Iniesta lazima utajuta.

Baada ya Guardiola kuumia Xavi akiwa mchezaji wa akiba, anapata nafasi na kuonesha kile alichonacho na moja kwa moja anajiandikia nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza.

Nini unaweza kuzungumza juu ya mchezaji huyu ambaye dunia yote kwa sasa inaendelea kumkumbuka zaidi?

# DONDOO

# CRYSTALA PALACE YAAMUA

LONDON, England


KLABU ya Crystal Palace iko kwenye mawindo ya kuinasa saini ya beki wa kati wa AC Milan, Strahinja Pavlovic.

Kwa mujibu wa ripoti, kocha wa Palace, Oliver Glasner, ndiye anayeshinikiza usajili wa mchezaji huyo.

## FLAMENGO YATAKA KIFAA

LONDON, England

KIUNGO wa kimataifa wa Italia, Jorginho, huenda akamalizana na mabosi wa klabu ya Flamengo ya Brazil. Kwa mujibu wa ripoti, Jorginho mwenye umri wa miaka 33, atatua Brazil mwishoni mwa msimu huu.



## SPURS YATAKA KUJIIMARISHA

LONDON, England

TOTTENHAM inaangalia uwezekano wa kuinasa saini ya mpachikaji mabao wa kimataifa wa Ufaransa, Eli Junior Kroupi.

Kwa mujibu wa ripoti, Tottenham inatoana jasho na klabu za Chelsea na West Ham United katika dili hilo.

## AL AHLI SASA YAKWAMA



NAPOLI, Italia

DILI la staa wa Al-Ahli ya Saudi Arabia, Allan Saint-Maximin, kujiunga na Napoli ya Italia limeonekana kukwama.

Kwa mujibu wa ripoti, klabu mbili hizo zimeshindwa kufikia makubaliano juu ya nyota huyo wa miaka 27.

## BRIGHTON IPO TAYARI




LONDON, England

KLABU ya Brighton inampigia hesabu mshambuliaji wa kimataifa wa Ugiriki anayekipiga PAOK, Stefanos Tzimas.

Kwa sasa, nyota huyo mwenye umri wa miaka 19 anakipiga kwa mkopo katika klabu ya Nurnberg.

## MAN UNITED YAMTOA UNDENDA



MANCHESTER, England

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ufaransa, Mathys Tel, amemwambia wakala wake kuwa anaitaka Manchester United.

Mazungumzo kati ya Man United na klabu yake ya Bayern Munich yamekwama, hivyo inasubiriwa kiangazi, mwaka huu.

SPORT MASTA



# DONGO!

## AMORIM AAMUA KUMTOLEA UVIVU MARCUS RASHFORD

MANCHESTER, England

MARCUS Rashford ambaye ameanza mazoezi rasmi ndani ya Aston Villa, siku chache baada ya kujiunga nayo akitokea Manchester United, amesema 'ameridhika' na sifa zote alizopewa na kocha wake wa zamani Ruben Amorim.

Amedai kwa sasa anapigana kupiga tizi la uhakika, kwani anaamini atakutana tu na Amorim siku si nyingi na kumdhihirishia ubaya wa maneno aliyozungumza juu yake.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England, alishutumiwa na kocha wake wa zamani Ruben Amorim kwa madai ni mvivu kuanzia mazoezini hadi kwenye mechi na hakuwa na msaada kwa timu.

Amorim alitoa kauli hiyo, mara tu baada ya Rashford kuondoka katika kikosi chake, huku mchezaji huyo akishangaa maneno yote hayo yametokea wapi.

"Rashford hakuwa msaada kwa timu, alikuwa mvivu, mzembe kuanzia mazoezini mpaka kwenye mechi, alitugharimua lakini namtakia mafanikio mema huko aendako," alisema Amorim.

Maneno hayo yanaonekana kumkwaza Rashford, ambaye ameendelea kudai anajua hana sifa hizo, lakini kwa kuwa amepewa hana budi kuzikubali na kuzifanyia kazi.

"Siwezi kubishana naye, sitaki kuingia huko, ila tutakutana tu uwanjani, nakubali sifa zote alizonipa," alisema Rashford huku akionekana mtu mwenye masikitiko makubwa.

Rashford alipambana kuondoka Manchester United na inadaiwa kurejea tena katika kikosi hicho itakuwa ngumu zaidi, pamoja na kutolewa huko kwa mkopo.




## KUNA KITU BADO KWA ARTETA

LONDON, England

IMEFICHUKA! Hatua ya aliyekuwa Mkurugenzi wa ufundi wa Arsenal, Edu, kuondoka ilitokana na kocha Mikel Arteta kupewa 'sauti ya mwisho' katika kuamua baadhi ya mambo, yakiwamo ya usajili wa wachezaji.

Edu, mchezaji wa zamani wa Arsenal aliyeanza ukurugenzi wa michezo klabuni hapo mwaka 2019, ndiye aliyefanikisha usajili wa wachezaji muhimu kikosini, wakiwamo Declan Rice, Martin Odegaard na David Raya.

Sasa, kwa mujibu wa ripoti, mkataba mpya wa Arteta ulimpa kocha huyo nafasi kubwa ya kufanya maamuzi, hivyo wakati mwingine kuwa na nguvu kuliko Edu.

